



MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR

06/05/2026

TAARIFA KWA UMMA JUU YA BEI ZA MAFUTA KWA MWEZI MEI 2026

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) inatangaza Bei za Mafuta kwa Mwezi Mei 2026 zitakazoanza kutumika rasmi kuanzia Siku ya Alhamis, **Tarehe 07/05/2026**.

Bei za Mafuta kwa Mwezi wa **Mei 2026** ni kama zifuatazo:

| AINA YA MAFUTA | BEI YA MWEZI APRILI, 2026 (TZS/LITA) | BEI YA MWEZI MEI, 2026 (TZS/LITA) | TOFAUTI (TZS/LITA) | TOFAUTI ASILIMIA |
|----------------|--------------------------------------|-----------------------------------|--------------------|------------------|
| PETROLI | 3,500 | 3,820 | 320 | 9.14 |
| DIZELI | 3,500 | 3,850 | 350 | 10 |
| MAFUTA YA TAA | 3,500 | 3,850 | 350 | 10 |

Sababu za kuongezeka kwa Bei za Mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa kwa Mwezi Mei, 2026 ni kuongezeka kwa bei za ununuzi wa mafuta katika soko la Dunia pamoja na kuongezeka kwa gharama za uagizaji kutoka katika soko la Dunia hadi kufika Zanzibar.

IMETOLEWA NA KITENGO CHA UHUSIANO ZURA



+255 24 294 1190
S.L.P 2238



info@zura.go.tz
zura.go.tz



Makao Makuu ZURA
25 Barabara ya Julius Nyerere
70473 Mjini Magharibi, Maisara, Zanzibar